# Mada: Nafasi ya Serikali Katika Kuanzisha, Kuratibu na Kusimamia Huduma za Tiba Saidizi Nchini Tanzania



**Deogratius Ramale**

**Head of training and Development – ISSUP Tanzania**

INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# KUHUSU ISSUP TANANIA NA ISSUP GLOBAL

**ISSUP Tanzania**

- Jumuiya ya wataalam wa masuala ya dawa za kulevya tawi la Tanzania ilizinduliwa rasmi mwaka 2023.
- Ni daraja bora kati ya watoa na wapokea huduma zinazohusu dawa za kulevya.
- Mpaka sasa Jumla ya wataalam wa ISSUP Tanzania imefikia **358**
- **ISSUP** ni fursa ya kujifunza na kujumuika na wataalam mbali mbali duniani kote.

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter


**STEP ONE: www.issup.net**





**STEP TWO: Click Log in**




**STEP THREE: Apply Now**




**STEP FOUR: Access Free Courses**



# UTANGULIZI


- Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina wajibu wa kudumisha ustawi wa wananchi wake katika maeneo mbalimbali


- Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya ina wajibu wa kuratibu shughuli za kinga, tiba na utengamao nchini.


- Kwa sababu suala la uthibiti wa dawa za kulevya ni suala la kisekta, Mamlaka hufanya kazi kwa kushirikiana na wizara mbalimbali, wadau wa maendeleo na asasi za kiraia katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya.

# MIONGOZO YA KITAIFA

- Huduma za kinga, tiba na utengamao hutolewa kwa kufuata miongozo maalumu ya utoaji elimu na tiba juu ya tatizo la matumizi ya dawa za kulevya.




ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS
TANZANIA chapter

# TIBA SAIDIZI JUU YA URAIBU WA DAWA ZA KULEVYA

**Maana**

- ❖ Tiba saidizi ni afua tiba juu ya uraibu wa dawa za kulevya unaohusisha tiba zaidi ya moja (package of services) zinazolenga kumsaidia mtu mwenye uraibu kupata nafuu dhidi ya uraibu.

- ❖ Kwa Tanzania methadone hutolewa kama sehemu ya tiba saidizi ikiambana na afua nyingine za magonjwa na changamoto zinazo ambana na uraibu.
  - ❖UKIMWI
  - ❖Kifua Kikuu
  - ❖Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii
  - ❖Afya ya Akili
  - ❖Homa ya ini
  - ❖N.k kulingana na hali ya mgonjwa wakati huo

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter


# MFUMO WA USHIRIKIANO NA ASASI ZA KIRAIA

- ❖ DCEA imekuwa ikitoa fursa za ushirikiano kwa asasi za kiraia nchini katika kutekeleza jukumu la kinga, tiba na utengamao nchini.

- ❖ Aina/Kazi za asasi za kiraia
  - ❖ Zinazotoa elimu kinga pekee
  - ❖ Zinazotoa elimu na rufaa ya tiba
  - ❖ Zinazotoa elimu, rufaa ya tiba na msaada wa kisaikolojia na kijamii

- ❖ Asasi hizi huwezeshwa kwa mafunzo na miongozo sahihi ya utoaji huduma. Na baadhi huwezeshwa kifedha kupitia miradi mbalimbali inayosimamiwa na serikali.

# RAMANI YA TANZANIA IKIONESHA HUDUMA ZA TIBA NA UTENGAMAO




Nyumba za Upataji Nafuu

Kliniki za MAT

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# AFUA ZA KUWAREJESHA KWENYE JAMII WALIOPATA NAFUU

- Mamlaka ya Dawa za Kulevya imetekeleza afua za urejeshwaji wa kijamii kwa waliopata nafuu kwa kutoa elimu kwa jamii, kupunguza unyanyapaa, na kutoa ushauri nasihi endelevu.
- Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau imewawezesha waraibu waliopata kupitia mafunzo ya ufundi stadi na kuwaunganisha na fursa za kujiajiri ili kujitegemea kiuchumi.
- Kwa mwaka 2026, Mamlaka inatarajia kuimarisha afua hizi kwa kupanua huduma za aftercare, kuongeza ushiriki wa jamii, na kuimarisha uwezeshaji wa kijamii na kiuchumi kwa waliopata nafuu ya uraibu wa dawa za kulevya.

# AHSANTENI SANA

KVP-FORUM TANZANIA




# Mahitaji na Uzoefu wa Walengwa wa Tiba Saidizi (MAT)

**Mtazamo wa Jamii – PWUID**




**Mwasilishaji:**
Marineus Mutongore
Mwenyekiti - KVP Forum Tanzania


ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# KUHUSU KVP FORUM TANZANIA

- KVP Forum ni **mwavuli wa mashirika yanayoongozwa na KVP** nchini Tanzania
- Inawakilisha sauti za jamii zilizo katika hatari zaidi, ikiwemo PWUID
- Ilianzishwa mwaka **2018**
- Mwaka **2019** ilitambuliwa na kuidhinishwa rasmi na Serikali
- Ilizinduliwa na **Waziri wa Afya – Mh. Ummy Mwalimu**

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# UZOEFU WA WALENGWA

Walengwa wengi wanaona MAT ni huduma muhimu kwa maisha yao

MAT husaidia:

- Kupunguza matumizi hatarishi
- Kurudi na kubaki kwenye huduma za afya
- Kuleta uthabiti wa maisha ya kila siku

Uzoefu wa walengwa hutofautiana kulingana na:

- Kituo cha huduma
- Mtazamo wa mtoa huduma
- Mazingira ya jamii inayozunguka

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# VIKWAZO VYA KUPATA HUDUMA

- Hofu ya kunyanyaswa au kukamatwa njiani
- Umbali wa vituo na gharama za usafiri
- Sharti la kufika kliniki kila siku
- Kukosa msaada wa karibu kutoka kwa peers
- Baadhi ya walengwa huacha huduma kwa sababu ya mazingira, si kwa hiari

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# UMUHIMU WA HUDUMA RAFIKI KWA WATEJA

Huduma rafiki huongeza uaminifu kwa mfumo wa afya

Hupunguza kuacha huduma (drop-out)

Huongeza ufuasi wa matibabu

Huduma rafiki zinajumuisha:

- Lugha yenye heshima
- Faragha na usiri
- Kutohukumu wala kudhalilisha
- Ushirikishwaji wa peers/walengwa waliopitia MAT

INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS
TANZANIA chapter

# CHANGAMOTO ZA UNYANYAPAA & KUKUBALIWA

## Walengwa hukumbana na Unyanyapaa:

- Kwenye baadhi ya vituo vya huduma
- Katika jamii zinazowazunguka
- Kutoka kwa vyombo vya dola

## Kukosa Kukubaliwa kama binadamu wanaohitaji msaada - Matokeo yake:

- Walengwa kujificha
- Kuacha huduma
- Kupotea kwenye mifumo ya afya

# MAPENDEKEZO KWA WATOA HUDUMA

- Kuimarisha huduma rafiki zisizo na hukumu
- Kushirikisha peers na mashirika yanayoongozwa na PWUID
- Kutoa elimu ya haki kwa walengwa
- Kuboresha usalama wa wanaofika vituo vya MAT
- Kusikiliza mrejesho wa jamii kupitia CLM na majadiliano ya wazi

INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS
TANZANIA chapter

# HITIMISHO – UJUMBE WA JAMII

MAT inafanya kazi pale walengwa:

| Wanaheshimiwa | Wanalindwa | Wanasikilizwa |
| --- | --- | --- |

Huduma bora hujengwa **pamoja na jamii**, si juu ya jamii

Ushirikiano wa kweli huokoa maisha na kuimarisha mifumo ya afya

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# AHSANTENI

# TAASISI NA MTANDAO

## Mada: Nafasi ya Asasi na Mtandao Katika Kusaidia Walengwa wa Matibabu Saidizi




Damali Lucas

TaNPUD- Head of Programs


ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# MUHTASARI WA WASILISHO

1. Utangulizi
2. Kuwahusisha Jamii
3. Kusaidia mifumo wezeshi kwa walengwa
4. Utetezi na kuwaunganisha katika huduma
5. Kupunguza Vikwazo vya Huduma
6. Mafanikio na ya kujifunza

# UTANGULIZI

- Asasi za kijamii, mitandao ya jamii na mifumo ya msaada rika ina nafasi kubwa ya kusaidia mtu aliyepo katika matibabu ya uraibu.
- Ni daraja kati ya huduma za kitabibu na kijamii
- Inawezesha umadhubuti katika matibabu ya uraibu kwa kuangalia saikolojia-jamii, hisia,mahitaji ya kiutendaji na kusaidia ufuatizi mzuri wa matibabu na kupunguza kiwango cha kurudi katika matumizi ya dawa za kulevya.

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# KUHUSISHA JAMII

- Inahusu wale walioathiriwa na jambo kuelewa uhatarishi walionao, kuwahusisha katika kuitikia kwa vitendo vinavyokubalika

**Namna ya kuwahusisha**

- Kuwajengea uwezo na kuwawezesha (wafahamu lengo,mawasiliano,ushirikiano, kujitambua, utofauti na kuhusisha, uhamasishaji wa rasilimali
- Kuwafikia watu –
- Kufanya uhamasishaji wa elimu (mabadiliko ya kitabia, hatua za kupitia , kupunguza uhatarishi,

**Mchakato:**

- Ifahamu Jamii husika –muundo, mabadiliko, nguvu ya mahusiano,chanzo cha taarifa, Imani na utendaji, rasilimali zilizopo
- Fahamu tamaduni za kijamii na muktadha wa kisiasa –mila,tetesi, taarifa zisizo rasmi, woga, utendaji hatarishi, chagua afua.

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# KUSAIDIA MIFUMO WEZESHI KWA WALENGWA

1.Kusaidia kufikia matibabu

2.Huduma saidizi na msaada wa kijamii

3.Elimu-saikolojia na unasihi

4.Kupunguza Unyanyapaa

5.Kufanya utetezi

6.Usaidizi rika na mafunzo kazini

7.Ufuatizi na kudumu katika matibabu

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# UTETEZI NA KUWAUNGANISHA KATIKA HUDUMA

- Ushiriki mkubwa katika tiba na kudumu katika matibabu
- Kuongeza ufuatizi wa matibabu
- Kupunguza kiwango cha kurudi katika matumizi ya dawa za kulevya
- Kuboresha hali ya maisha na kupunguza uhalifu
- Kuleta matokeo mazuri ya afya ya akili

# KUPUNGUZA VIKWAZO VYA HUDUMA

- Daraja la kuondoa vikwazo vya kufikia huduma (serikali na asasi)
- Kuhamasisha utu na kupinga unyanyapaa (kuzuia/kupunguza maneno ya aibu, vitendo ukatili, usumbufu, unyanyasaji,
- Kuwa mtaji wa upataji nafuu (mfano: mafunzo ya ufundi stadi, nyumba za upataji nafuu, kuzuia kurudi katika matumizi
- Kuwa na uzoefu na msaada rika –wataalamu rika wa upataji nafuu, hakuna hukumu,inajenga uaminifu, kuna ushirikeli
- Kuwahusisha wengine katika safari ya upataji nafuu –familia, wenza, marafiki
- Uhamasishaji wa sera za utetezi –sera rafiki juu ya tiba, na mbadala wa kifungo

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS
TANZANIA chapter

# MAFANIKIO NA YA KUJIFUNZA

1.Kuwa na matibabu,
2.Thibitisha,
3.Kusambaza mazuri ya kujifunza,
4.Kuboresha ufanisi wa matibabu na sera

INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS
TANZANIA chapter

# AHSANTENI

# UTANGULIZI




**Jina:Saidi John Bandawe.**

***Nafasi: Katibu Mtendaji na Mjumbe Mwanzilishi kutoka Gift of Hope Foundation, Mtaalamu wa Msaada wa Upataji nafuu , Mtaalamu wa Kinga pia ni Mkufunzi Rika anae pata nafuu .***

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# MUHTASARI WA WASILISHO

1. Utangulizi
2. Msaada wa Upataji nafuu kutoka kwa muelimishaji rika ndani ya tiba saidizi.
3. Umuhimu wa waelimishaji rika
4. Jinsi muelimishaji rika anavosaidia uzingatiaji
5. Kujenga uaminifu na walengwa
6. Safari ya urejeaji na uhamasishaji
7. Changamoto za maeneo ya kazi
8. Hitimisho

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# MSAADA WA UREJEAJI KUTOKA KWA MUELIMISHAJI RIKA NDANI YA TIBA SAIDIZI

- Msaada wa upataji na na tiba unafanya kazi pale kundi rika linapo shiriki katika kutoa huduma na watu wenye uzoefu ambao wanaweza kuwasaidia wengine kuanza safari ya upataji nafuu ,kuendelea kubaki katika tiba na kuwa na maisha bora binafsi na kifamilia katika upataji nafuu wa muda mrefu.
- Huduma hizi ni aina ya msaada wa kijamii unaotolewa na wataalamu wa msaada wa kundirika wanapata nafuu.
- Wataalamu wa msaada wa upataji nafuu ni waelimishaji rika ni nguzo muhimu katika jitihada za watu kuishi na au kuendelea kupata nafuu kutoka kwenye matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya na vilewesho .
- Uelimishaji rika ni mfumo wa utoaji huduma kwa kutumia muelimisharika ambaye ni miongoni walengwa/aliyekuwa mmoja wa kundirika.

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# UMUHIMU WA WASAIDIZI RIKA

**Wasaidizi wa rika na huduma -** Kuwatambua, kuwahamasisha na kuwapa walengwa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya

- Kutoa huduma ya uelimishaji kwa jamii na mitandao ya watumiaji wa dawa za kulevya
- Kugawa vipeperushi na upimaji na kujikinga na magonjwa ambukizi .
- Kuwasaidia kupata msaada na rasilimali
- Kuchangia uzoefu wao
- Kutoa taarifa za msaada wa kijamii
- Kusaidia kujenga uhusiano na ujuzi wa upataji nafuu
- Kutoa ushauri na rufaa mbalimbali
- Kusaidia kuweka malengo
- Kuwa kiunganishi cha taarifa kati ya familia ,watoa huduma na mpotokea huduma
- Maandalizi katika Asasi za Kiraia ambapo mtu mwenye uraibu hupewa elimu ya afya, Elimu juu ya tiba na huduma nyingine tegemezi,

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# JINSI MUELIMISHAJI RIKA/MSAIDIZI RIKA ANAVYOSAIDIA UZINGATIAJI

- Kutambua maeneoe ya kutolea huduma ngazi ya jamii na vituo vya huduma
- Kufanya mazungumzo ya awali na mpatiwa huduma na kupanga mpango kazi jumuishi.
- Kufuatilia mabadiliko ya tabia za walengwa
- Kutoa rufaa na kuwasindikiza walengwa kupata huduma mbalimbali
- kuhakikisha rufaa zimepokelewa na kurudisha mrejesho.
- Kusimamia sheria na taratibu za tiba ya methadone katika kliniki
- Kufuatilia ufuasi mzuri wa tiba
- Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi na changamoto kwa ajili ya huduma
- Kuielezea huduma kikamilifu kwa watumiaji wa dawa za kulevya pamoja na faida zake
- Kuwasikiliza kwa umakini, uwazi na kuheshimu mawazo ya watumiaji wa dawa za kulevya
- Kuruhusu kuulizwa maswali juu ya huduma watakazozipata

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# KUJENGA UAMINIFU NA WALENGWA

- Mbinu za mawasiliano na kuomba ruhusu ya kutoa taarifa ya mpatiwa huduma.
- Mfano wa kuigwa na nidhamu, kujitoa na heshima
- Anajiamini ,msirina kujituma kwenye kazi
- Awe amepata au apewe mafunzo ya uelimishaji rika
- Kuielezea huduma kikamilifu kwa watumiaji wa dawa za kulevya pamoja na faida zake
- Kuwasikiliza kwa umakini, uwazi na kuheshimu mawazo ya watumiaji wa dawa za kulevya
- Kuruhusu kuulizwa maswali juu ya huduma watakazozipata
- Kutoa elimu katika muundo wa ushirikishwaji
- Kumuona kwanza mkuu wa kaya wa maskani kwa ajili ya kujitambulisha na kukaribishwa
- Kutembea na vitambulisho pamoja na vibali vya kazi
- Kuangalia muda muafaka wa kuwaona walengwa maskani ili kuwapata kwa ajili ya kuwapa huduma lakini pia kuzingatia usalama

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# SAFARI YA UREJEAJI NA UHAMASISHAJI

- **Usaidizi Upataji Nafuu wa kujitolea kati ya rika na rika**, zinazotolewa na programu za hatua 12 (12-step programs) na programu nyingine za kijamii za kusaidiana, zimesaidia watu wengi wanaopona au wanaotafuta kupona kutokana na uraibu (SUD) muda mrefu kabla ya kuanzishwa kwa mfumo rasmi wa PRSS .
- **Programu za Matibabu ya Uraibu (SUD)** – Rika hutoa usaidizi wa mtu binafsi, familia, au kikundi, wakitoa mtazamo wa kipekee kama mtu ambaye pia amepambana na uraibu na sasa yuko kwenye hatua ya kupona.
- **Hospitali** – Rika hutoa usaidizi wa kihisia na kuunganisha wagonjwa na huduma muhimu, ikiwa ni pamoja na matibabu ya uraibu.
- **Mashirika ya Jamii Yanayoendeshwa na Rika** – Rika huongoza vikundi vya usaidizi, kutoa elimu ya upataji nafuu (recovery coaching), au huduma nyingine za kusaidia watu kudumisha hali yao ya upataji nafuu na kurejea kikamilifu katika jamii zao.
- **Nyumba za Upataji Nafuu (Recovery Housing)** – Hurejelea mazingira salama, yenye afya, na yasiyo na matumizi ya kulevya ambayo husaidia watu wanaopona uraibu. Mara nyingi, nyumba hizi husimamiwa na rika ili kudumisha mazingira yenye mpangilio na usaidizi.
- **Mazingira ya Haki ya Jinai** – Wataalamu Rika wa upataji nafuu hutoa huduma za usaidizi kwa watu walio katika mfumo wa haki ya jinai, kama vile wale walio katika mahakama za dawa za kulevya au magerezani.
- **Mazingira ya Kazi au Elimu** – Baadhi ya waajiri au vyuo hutoa huduma za upataji nafuu kama sehemu ya programu zao za ustawi wa wafanyakazi na wanafunzi.
- **Kupitia Teknolojia** – Kutokana na kukua kwa huduma za afya kwa njia ya simu (telehealth) na vikundi vya usaidizi vya mtandaoni, huduma za upataji nafuu sasa zinaweza kutolewa kupitia majukwaa ya kidijitali.

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# CHANGAMOTO NA UZOEFU WA KAZI

- Upungufu wa wataalam walipata mafunzo ya upataji nafuu .
- Ufinyu wa bajeti na ukosefu ya mafunzo na kufikia wapatiwa huduma wengi zaidi
- Wanawake wanaotumia dawa za kulevya kujitokeza kupata huduma.
- Wafaidika wanakua na changamoto zaidi ya dawa za kulevya ,Afya,Sheria na Familia.
- Jamii haitambui tatizo la uraibu hii imeleta unyanyapa na ubaguzi.
- Wapatiwa huduma kuto fata mwongozo na taratibu za kliniki/ vituo vya afya vinavyotoa huduma na tiba ya Methadone na tiba zingine ,kuachana na huduma.
- Kutokuwa na Maarifa kuhusu Kanuni za Maadili kwa Wataalamu wa Usaidizi wa Upataji Nafuu
- Mipango ya udhibiti wa msongo wa mawazo na uchovu wa kupitiliza, na hatua za kujijali
- Ukosefu wa maarifa kuhusu Mtaala wa Kimataifa wa Upataji Nafuu (URC)

# NINI KIFANYIKE KWA MAKUNDI RIKA

- Kanuni za Maadili kwa Wataalamu wa Usaidizi wa Upataji Nafuu: huainisha tunu za kimsingi na misingi ya utendaji wa usaidizi wa rika. Kanuni hizi hutumika kama mwongozo kwa Wataalamu wa Usaidizi wa Kupona.
- Wajibu wa kitaalamu na viwango vya maadili kwa ajili ya taaluma hii vimefafanuliwa hapa ndani.
- Wataalamu wa Upataji nafuu wana wajibu wa kumsaidia mtu mwenye uraibu wa dawa za kulevya kwa kumtambua, kupanga na kufikia malengo binafsi ya upataji nafuu.

**Mapitio ya Mafunzo na Usimamizi**

- Kupitia maudhui ya mafunzo na kuyafanyia mabadiliko ya lazima kwa ajili ya kuimarisha ubora wa kifurushi cha mafunzo ambacho kitatumiwa katika mafunzo yajayo.
- Ziara ya ushauri na uelekezi (mentorship) itafanyika katika jamii na Mashirika ya Kiraia (CSO) ili kusaidia timu kuanzisha huduma zinazozingatia viwango vinavyohitajika.
- Anzisha Mfumo wa Nguvu Rika Ya Uzoefu katika Upataji nafuu

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS
TANZANIA chapter
ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

# MWISHO

# AHSANTENI

# KINGA NA TIBA SAIDIZI

# Mada: Kinga na Tiba Saidizi:Nafasi Ya Kinga katika Mfumo wa Matibabu



**Imeandaliwa na**

**Surah Nyembo**

**Recovery support professional**

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# MUHTASARI WA WASILISHO

1. Utangulizi
2. Kinga katika Kuendelea na Matumizi ya Vilevi
3. Afua za Awali na Kupunguza Hatari
4. Nafasi ya Elimu na Uhamasishaji
5. Kupunguza Unyanyapaa kupitia Kinga
6. Safari ya urejeaji na uhamasishaji
7. Jinsi kinga inavyosaidia matokeo ya Tiba
8. Hitimisho

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS TANZANIA chapter

# KINGA YA KUENDELEA NA MATUMIZI YA VILEVI

- Inahusu mbinu mbalimbali inayotegemea ushuhuda ili kupunguza hatua za hatari kuongezeka kutoka mtu asie anza kutumia,anaetumia kwa majaribio,mtumiaji wa mara kwa mara mpaka mtegemezi au mraibu.
- Mikakati ya kinga imepangwa kulingana na hatua za matumizi

i. Mtu asiye tumia ina lenga asiingie katika utumiaji.

ii. Mtu aliye katika majaribio inalenga kuto endelea na tabia hatarishi.

iii. Mtumiaji wa mara kwa mara ina lenga uingiliaji kati mapema na kuto pata madhara.

iv. Mtegemezi ina lenga matibabu,kupunguza madhara na kupata nafuu.

# AFUA ZA AWALI NA KUPUNGUZA HATARI

- Mikakati ya kinga katika wigo wa uingiliaji kati umegawanyika kulingana na idadi ya watu wanaolengwa na kiwango cha hatari

i. Kinga ya wote – inalenga idadi ya watu kiujumla mf: (program za mashuleni na uhamasishaji umma).Hii husaidia kuzuia kuanza kutumia.

ii. Kinga teule- inalenga vikundi vidogo vilivyo katika hatari kubwa mf: Watoto wa watumiaji wa dawa za kulevya na vijana waliopo kwenye maeneo yenye uhalifu mwingi.

iii. Kinga iliyoonyeshwa- inalenga walio jaribu dawa za kulevya au kuonesha dalili za mapema za matumizi mabaya ili kuzuia kuwa wategemezi/waraibu.

# VIPENGELE MUHIMU VYA KINGA

- Ushuhuda umekuwa kipengele muhimu kwenye kinga na umeleta ufaulu mkubwa katika jamii.
- Watoa huduma ya kinga wanatakiwa kuwa na mpango mkakati ili kufanya huduma iendelee pia kujidhatiti hasa mashuleni na kuweka mahusiano na familia za vijana ambao wapo katika shinikizo rika.
- Sera na mabadiliko ya mazingira itakayo husisha udhibiti katika upatikanaji wa vitu kama pombe
  i. Kupitia kodi
  ii. Mipaka ya umri
  iii. Vikwazo vya matangazo

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS
TANZANIA chapter

# MALENGO YA KINGA

- Kinga ya msingi-kuzuia  kuanza matumizi.
- Kinga ya sekondari-Utambuzi wa mapema na uingiliaji kati ili kuzuia. kuendelea na matumizi
- Kinga ya juu-matibabu ya utegemezi ili kuzuia madhara na kurudia tena.

# AFUA ZA AWALI NA KUPUNGUZA HATARI

- Afua ni kama Daraja la kinga na tiba
- Afua inaweza kufanyika kwa njia ya uchunguzi(screening), afua fupi na rufaa Kwenda katika matibabu .
- Njia hii husaidia kupunguza hatari kwa yule ambaye ameanza kutumia dawa za kulevya,afua itamsaidia asiwe mtegemezi.
- Lakini pia humsaidia mraibu kupata matibabu mengine nje ya uraibu.
- Kiufupi huondoa hatari kwa walioanza dawa za kulevya au wategemezi mf: Afua kwa  dereva anaye tumia dawa za kulevya au yule mama mjamzito anayetumia dawa za kulevya.

# ELIMU NA UHAMASISHAJI

**Umuhimu wa Elimu na Uhamasishaji:**

i. Kuzuia (Prevention): Elimu mashuleni na katika jamii hufundisha kuhusu hatari za matumizi ya dawa za kulevya, na hivyo kuzuia watu kuanza.

ii. Kupunguza Unyanyapaa: Uhamasishaji husaidia jamii kuelewa kuwa uraibu ni ugonjwa na sio udhaifu wa kimaadili, hali inayowafanya waathirika kutafuta msaada.

iii. Kutambua Dalili Mapema: Watu huelimishwa kutambua dalili za awali za uraibu, jambo linalowezesha kuingilia kati na kutoa msaada mapema.

iv. Kuhimiza Matibabu: Uhamasishaji hutoa taarifa kuhusu vituo vya matibabu, ushauri nasaha, na mbinu za kupata nafuu.

v. Kujenga Matumaini: Kushirikisha watu waliopata nafuu kuonyesha kuwa kupata nafuu kunawezekana, na kuwapa moyo wanaopambana na uraibu.

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

# KUPUNGUZA UNYANYAPAA

- Lugha na mawasiliano- itumike njia ya lugha na mawasiliano isiyo hukumu na inayo tegemea sayansi mf: mraibu utamwita mtu mwenye tatizo la matumizi ya dawa za kulevya.
- Elimu na uelewa – kuongeza uelewa juu ya uraibu mashuleni,mahala pa kazi,na kwenye jamii ili kuondoa hadithi potofu.
- Mawasiliano ya kijamii- inatakiwa kukuza fursa za mwingiliano na watu wenye uzoefu wa moja kwa moja kama program saidizi zinazoongozwa na rika lakini pia na matukio ya kijamii.
- Utetezi wa sera- ni vyema kutekeleza sheria na sera za kupinga ubaguzi katika maeneo ya kazi na  mazingira ya huduma za afya .

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS

ISSUP INTERNATIONAL SOCIETY OF SUBSTANCE USE PROFESSIONALS
TANZANIA chapter

# KUPUNGUZA UNYANYAPAA

- Uwezeshaji- ni vyema kusaidia na kurekebisha kwa kutafuta matibabu na kuhimiza upataji nafuu badala ya kunyanyapaa.
  - Tujitahidi kutoa elimu sahihi kwa umma na huduma saidizi ili kupunguza unyanyapaa

# UMUHIMU WA KINGA KATIKA MATIBABU

- Husaidia matibabu.
- Kugundua na kuanza afua mapema.
- Huwezesha rufaa kwa wakati.
- Hupunguza maambukizi ya magonjwa (VVU/Homa ya Ini C).
- Kiungo kati ya watu na huduma za matibabu ya uraibu.
- Husaidia watu kutorudi katika utegemezi wa vilevi.
- Hupunguza vihatarishi(matibabu makubwa).

# AHSANTENI